



Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 (0)22-2122722/3
Nukushi: +255 (0)22-2130852
Barua pepe: dg@nbs.go.tz
Tovuti: www.nbs.go.tz

18 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 796,
11992 - Dar es Salaam
TANZANIA.



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb Na: NBS/S.40/21/534

YALIYOJITOKEZA

Tarehe: 08 Machi, 2018

FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KWA MWEZI FEBRUARI, 2018

MAELEZO YA MBINU NA KANUNI ZA UKOKOTOAJI FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA

Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za Bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na sampuli wakilishi ya kaya binafsi nchini Tanzania. Bei za bidhaa na huduma 278 zikiwa ni pamoja na bidhaa 97 za Vyakula na Vinywaji Baridi na 181 zisizo za Vyakula hukusanywa kila mwezi katika kila mkoa.

Mizania Mpya za Bidhaa na Huduma na Jamii na Kizio cha Bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 25 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijiji yaliyotokana na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya binafsi wa mwaka 2011/12. Kizio cha bei kinachotumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa ni cha mwezi Desemba, 2015.

Makundi ya Bidhaa na Huduma za Jamii

Fahirisi za Bei za Taifa hufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi za Bei zinajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi-vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za Bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

Namna ya Kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Kuna maboresho mengi yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric mean of Price Relatives" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo; matumizi ya mfumo ulioboreshwu wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Mbinu na kanuni ya Lowe Index Formula ambayo ni aina ya "Laspeyres Index Formula" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEONGEZeka HADI ASILIMIA 4.1

Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Februari, 2018

(Des., 2015 = 100)

Na. .	KUNDI (MAIN GROUP)	Mizania (Weight)	Feb -17	Jan -18	Feb -18	Badiliko la mwezi mmoja	Badiliko la miezi 12
1	Vyakula na vinywaji baridi	38.5	111.16	115.51	117.18	1.4	5.4
2	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	3.7	105.54	107.89	107.94	0.0	2.3
3	Mavazi ya nguo na viatu	8.3	104.33	107.15	107.82	0.6	3.3
4	Nishati, Maji na Makazi	11.6	112.67	119.12	122.35	2.7	8.6
5	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	6.3	104.18	105.71	105.88	0.2	1.6
6	Gharama za Afya	2.9	105.35	107.01	107.03	0.0	1.6
7	Usafirishaji	12.5	99.72	100.58	101.36	0.8	1.6
8	Mawasiliano	5.6	98.46	98.09	98.24	0.2	-0.2
9	Utamaduni na Burudani	1.6	101.57	103.07	103.07	0.0	1.5
10	Elimu	1.5	103.00	105.34	105.55	0.2	2.5
11	Hoteli na Migahawa	4.2	104.27	105.01	105.25	0.2	0.9
12	Bidhaa na huduma nyinginezo	3.1	102.93	105.66	105.74	0.1	2.7
JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE		100.00	106.97	110.13	111.33	1.1	4.1

Makundi Mengine Teule

1	Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa nyumbani na mahotelini	37.07	111.88	116.63	118.33	1.5	5.8
2	Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika nyumbani pamoja na petroli na dizeli	8.68	115.44	124.76	129.40	3.7	12.1
3	Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula	62.93	104.56	106.99	107.98	0.9	3.3
4	Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, nishati na mafuta	54.25	102.82	104.14	104.55	0.4	1.7

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali Namba 1 hapo juu linaonesha kuwa, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwezi Februari, 2018 umeongezeka kidogo hadi asilimia 4.1 kutoka asilimia 4.0 mwezi Januari, 2018. Hii inamaanisha kuwa, kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Februari, 2018 imeongezeka ikilinganishwa na kasi ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Januari, 2018. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 111.33 mwezi Februari, 2018 kutoka 106.97 mwezi Februari, 2017. Mfumuko wa Bei wa bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi kwa mwezi Februari, 2018 umepungua hadi asilimia 5.4 kutoka asilimia 6.3 ilivyokuwa mwezi Januari, 2018.

Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula


Mfumuko wa Bei kwa kipimo cha mwaka kwa bidhaa za vyakula nyumbani na migahawani kwa mwezi Februari, 2018 umepungua hadi asilimia 5.8 kutoka asilimia 6.7 mwezi Januari, 2018. Aidha, badiliko la Fahirisi za Bei kwa bidhaa zisizo za vyakula kwa mwezi Februari, 2018 limeongezeka hadi asilimia 3.3 kutoka asilimia 2.8 mwezi Januari, 2018.

Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma zote isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi Februari, 2018 umeongezeka kidogo hadi asilimia 1.7 kutoka asilimia 1.4 mwezi Januari, 2018.

Fahirisi inayotumika kukokotoa aina hii ya Mfumuko wa Bei, hajumuishi vyakula vinavyoliwa nyumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa, kuni na umeme. Vyakula na bidhaa za nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara, hivyo vikiondolewa kwenye fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera.

Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mwezi Februari, 2017 hadi Februari, 2018. (Des. 2015 = 100)



Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonesha kuwa, Fahirisi za Bei zimekuwa na mwenendo imara kutoka mwezi Februari, 2017 hadi mwezi Februari, 2018. Katika kipindi hicho, Mfumuko wa Bei nao umekuwa na mwenendo imara kutoka asilimia 5.5 mwezi Februari, 2017 hadi asilimia 4.1 mwezi Februari, 2018.

MABADILIKO YA FAHIRISI ZA BEI KATI YA MWEZI JANUARI, 2018 NA MWEZI FEBRUARI, 2018.

Fahirisi za Bei kati ya mwezi Januari, 2018 na mwezi Februari, 2018 zimebadilika kwa asilimia 1.1 ikilinganishwa na badiliko la asilimia 0.8 ilivyokuwa kati ya mwezi Disemba, 2017 na mwezi Januari, 2018. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 111.33 mwezi Februari, 2018 kutoka 110.13 mwezi Januari, 2018. Kuongezeka kwa Fahirisi za Bei kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa fahirisi ni pamoja na; viazi vitamu kwa asilimia 8.1, mihogo kwa asilimia 4.6, mbogamboga kwa asilimia 3.8, mahindi kwa asilimia 3.5, njegere kwa asilimia 3.5 na ndizi za kupika kwa asilimia 2.3.

Kwa upande mwingine bidhaa zisizo za chakula zilizochangia kuongezeka kwa fahirisi za bei ni pamoja na mkaa kwa asilimia 4.4, petrol kwa asilimia 2.3, dizeli kwa asilimia 2.1, na mavazi ya wanaume kwa asilimia 1.5.

Jedwali Namba 2: Shajala ya Fahirisi za Bei za Taifa kwa Miezi Ijayo

Fahirisi za Bei za Taifa	Tarehe ya Toleo
Machi, 2018	9 th Aprili, 2018
Aprili, 2018	8 th Mei, 2018
Mei, 2018	8 th Juni, 2018

Kwa mawasiliano zaidi tafadhali wasiliana na:

Mkurugenzi Mkuu,
Ofisi ya Taifa ya Takwimu
18 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 796
11992 - Dar es Salaam
TANZANIA.

Simu: +255 (0)22-2122722/3
Nukushi: +255 (0)22-2130852 ,
Barua pepe: dg@nbs.go.tz
Tovuti: www.nbs.go.tz